# Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

## Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)

# Matukio ya Wiki

Kitengo cha Habari na Masoko, MUCE

*Tarehe 1 Agosti - 30 Septemba 2022*






## Yaliyomo


- Ziara ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Iringa | Uk. 1
- Mafunzo ya usimamizi wa wanafunzi wa uzamili kwa kutumia ARIS 3 | Uk. 2
- Semina ya zoezi la usimamizi wa wanafunzi kwa vitendo 2022 | Uk. 3
- Mwenge wa Uhuru Iringa | Uk. 4
- Machapisho | Uk. 5 - 6
- Wafanyakazi waliopanda vyeo na wafanyakazi wapya | Uk. 7 - 10
- Hafla ya kumkaribisha chuoni Mkwawa Naibu Rasi - Taalam, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam | Uk. 11 - 12

# ZIARA YA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN MKOANI IRINGA





Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Halima Dendego

Chuo kilishiriki kwenye ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, mkoani Iringa iliyofanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe 11 hadi 13 Agosti 2022. Kwenye ziara hiyo, Chuo kupitia Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Iringa, Dr. Abel Nyamahanga, kilimshukuru Mhe. Rais pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ufadhili wa dola za kimarekani 8,000,000 kutoka Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET). Fedha hizo zitakisaidia Chuo kuboresha mazingira ya utendaji kazi, kusomesha wanataaluma na kuandaa programu zinazoendana na soko la ajira.



Rasi wa Chuo, Prof. Esther W. Dungumaro (wa pili kutoka kushoto) na viongozi wengine wa Serikali







# MAFUNZO YA USIMAMIZI WA WANAFUNZI WA UZAMILI KWA KUTUMIA ARIS 3

Chuo kupitia Kurugenzi ya Shahada za Uzamili iliendesha mafunzo ya usimamizi wa wanafunzi wa shahada za uzamili kwa kutumia mfumo wa ARIS 3 yaliyofanyika tarehe 25 na 26 Agosti 2022 chuoni Mkwawa. Mafunzo hayo yaliwezeshwa na Prof. Donatha Tibuhwa – Mkurugenzi wa Shahada za Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kampasi ya Mwalimu Nyerere, kwa kushirikiana na watalaam wa mfumo wa ARIS 3, Bw. Solomon Aridy na Bw. Victor Mataba na Afisa Tawala Mwandamizi katika Kurugenzi ya Huduma kwa Umma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bi. Noela Jonathan.

# SEMINA YA USIMAMIZI WA WANAFUNZI KWENYE MAFUNZO KWA VITENDO, 2022



Tarehe 1 Septemba 2022 ilifanyika semina ya usimamizi wa wanafunzi kwenye mafunzo kwa vitendo kwa mwaka 2022. Semina hiyo iliandaliwa na Ofisi ya Mratibu wa Mafunzo kwa Vitendo na kuwezeshwa na Dkt. John Kalolo, Bw. Willy Kasuga, Dkt. Vicent Jalang'o, Dkt. Orestes Kapinga, Dkt. Mariana Mhewa na Bw. Edward Nsolo. Zoezi la mafunzo kwa vitendo linafanyika kuanzia tarehe 5 Septemba hadi 14 Oktoba 2022.





Rasi wa Chuo, Prof. Esther W. Dungumaro na walimu wa Shule ya Sekondari Kimaseki - Arusha (Godwin Philipo - wa kwanza kulia na Abdallah Suleiman), ambao pia ni wahitimu wa MUCE 2006-2009. Rasi wa Chuo alitembelea Shule hiyo kwa ajili ya zoezi la mafunzo kwa vitendo na tafiti fuatilizi.



# MWENGE WA UHURU IRINGA

Chuo kilishiriki mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kati ya Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Morogoro yaliyofanyika tarehe 2 Septemba 2022 katika Kijiji cha Mapanda kilichopo Wilaya ya Mufindi. Mbio za Mwenge zinalenga kukagua shughuli za maendeleo na kumulika miradi mbalimbali ili kuleta mshikamano, umoja na tija kwa Taifa.










# Machapisho

**Hongera sana wanataaluma wafuatao kwa kutoa machapisho kwenye majarida mbalimbali ya kimataifa.**

Biasazin, T. D., Herrera, S. L., **Kimbokota, F.** and T. Dekker (2022). Diverging olfactory sensitivities to yeast volatiles reflect resource partitioning of tephritids and drosophilids. *Ecology and evolution*. DOI: 10.999762. doi:10.3389/fevo.2022.999762.

Chacha S. C. (2022). On solution and perturbation estimates for the nonlinear matrix equation XA^{*} e^{X} A= I  X-A∗ e XA= I. *Journal of the Egyptian Mathematical Society*, 30(18). DOI: https://doi.org/10.1186/s42787-022-00152-z.

Fussy, D. S., and Iddy, H. (2022). Literacy practices as an arena for girls' development of literacies. *Education Inquiry*, DOI: 10.1080/20004508.2022.2112526.

**Lwiwa C. B.** and Nydal O. J. (2022). 3D ray tracing for optimizing a mirror tiled compound parabolic concentrator. *16th Conference on heat transfer fluid mechanics and thermodynamics*, pp 16–22.

Khan, H. **Hazina, C**., Lee, C. S. (2022). Synergistic effect stemming from vertically anchored seamless 2D MoSe2 nanosheets on 1D NiTiO3 nanofibers toward CO2 photoreduction. *Journal of CO2 Utilization*, 61, 102058. DOI: https://doi.org/10.1016/j.jcou.2022.102058.

**Mafwele, B**. J. and Lee, J. W. (2022). Relationships between transmission of malaria in Africa and climate factors. *Scientific Reports*, DOI: https://doi.org/10.1038/s41598-022-18782-9.

Mketo, A. R., Ringo, C. J., Nuhu, S., and **Mpambije, C. J.** (2022). Enhancing community participation for environmental health improvement in rural Tanzania: Evidence from Bukombe district. *Evaluation and Program Planning*, DOI: 10.1016/j.evalprogplan.2022.102152.

**Mkupete, J. M.**, Fintel, D. V., and Burger, R. (2022). Decomposing inequality of opportunity in child health in Tanzania: *The Role of Access to Water and Sanitation*, 41(2): pp. 99-111.

# Machapisho


Msokwe, D. and **Mulungu, C. D.** (2022). The use of Family Planning Methods (FPMs) in Ilala Municipality, Dar Es Salaam, Tanzania. *Ghana Journal of Geography*, 14(2), pp. 82-106.

**Mng'ong'o, B. G.,** Rad, D., Koloseni, D. and Balas V. E. (2022). Application of fuzzy TOPSIS assessing performance of agro-processed organic crops: A case of Sustainable Agriculture Tanzania (SAT) in Morogoro. *Journal of Intelligent & Fuzzy System*, 43(2), pp. 1811-1826.

**Ndomondo, E.**, Mbise, A., and Katabaro, J. (2022) History teachers' conceptualization of competency-based curriculum in transforming instructional practices in lower secondary schools in Tanzania. *Social Sciences & Humanities Open*, 6, pp. 1–9.

**Ngao, A**. I., Sang, G., and Kihwele, J. E. (2022). Understanding Teacher Educators' Perceptions and Practices about ICT Integration in Teacher Education Program. *Educ. Sci.*, 12, 549. DOI: https://doi.org/10.3390/ educsci12080549.

Sanga, V. F., Fabian, c. and Kimbokota, F. (2022). Heavy metal pollution in leachates and its impacts on the quality of groundwater resources around Iringa Municipal solid waste dumpsite. *Environmental Science and Pollution Research*, DOI: https://doi.org/10.1007/s11356-022022760-z.

**Wakati, M.**, Vuzo, M., and **Kapinga. O.** (2022). English Language Teachers' Assessment Practices of Oral Language Skills in Secondary Schools in Tanzania. *Journal of Linguistics and Language in Education*, 16(1), pp. 64–90.

# Wafanyakazi waliopanda vyeo

*Wafanyakazi wanataaluma wanne wamepandishwa vyeo kutoka Wahadhiri kwenda Wahadhiri Waandamizi kutokana na kupata alama zinazohitajika kwenye makala na ufundishaji. HONGERENI SANA NA KILA LA HERI KWENYE MAJUKUMU YENU MAPYA.*



Dkt. Selina Thomas Mkimbili

**Mhadhiri Mwandamizi**
**Idara ya Saikolojia ya Elimu na Taaluma za Mitaala**



Dkt. Hassan Iddy Hassan

**Mhadhiri Mwandamizi**
**Idara ya Saikolojia ya Elimu na Taaluma za Mitaala**



Dkt. Fransisco Paul Mugizi

**Mhadhiri Mwandamizi**
**Idara ya Jiografia na Uchumi**



Dkt. Japhace Balwegilila Poncian

**Mhadhiri Mwandamizi**
**Idara ya Historia, Sayansi ya Siasa na Taaluma za Maendeleo**

# Wafanyakazi waliohamia MUCE



Tobias T. Nyoni

Mwangalizi wa Wanafunzi Daraja la II



Ezekia E. Wikedzi

Mwangalizi wa Wanafunzi Daraja la II



Gloria M. Spotwa

Mwangalizi wa Wanafunzi Daraja la II



Sifael J. Samson

Mwangalizi wa Wanafunzi Daraja la II



Rahel M. Mwigo

Mwangalizi wa Wanafunzi Daraja la II



Ndigwako J. Sangabo

Muuguzi



Oscar I. Mbwale

Mtabibu Daraja la II



Joyce F. Sossiya

Mtabibu Daraja la II



Kelvin N. Neckemiah

Mtabibu Daraja la II



Beatrice K. Paul

**Mtunza Kumbukumbu Msaidizi Daraja la I**



Gaston G. Ndunguru

**Afisa Tawala Daraja la I**



Aggrey M. Manga

**Afisa Tawala Daraja la I**



Ramadhan I. Mwinyi

**Afisa Ununuzi Daraja la II**



Mathayo S. Rumas

**Mhasibu Daraja la II**



Grace M. Wambura

**Mhasibu Daraja la II**



Lewis F. Madaba

**Mhasibu Mwandamizi**



Samwel R. Madale

**Mnukuzi wa Nukta Nundu Daraja la I**



Patrick J. Mizimu

**Mwanasheria Daraja la II**



Charles D. Maulaga

**Afisa TEHAMA Mwandamizi Daraja la II**

# Karibu MUCE

## *Prof. Deusdedit A. Rwehumbiza*

**Naibu Rasi - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam**



Tarehe 12 Septemba 2022 ilifanyika hafla ya kumkaribisha chuoni Mkwawa Naibu Rasi - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Deusdedit A. Rwehumbiza, iliyohudhuriwa na viongozi wa Chuo. Prof. Deusdedit A. Rwehumbiza aliteuliwa kuwa Naibu Rasi - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam tarehe 6 Septemba 2022 na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Deusdedit A. Rwehumbiza ni Profesa Mshiriki kwenye Idara ya Menejimenti, Shule Kuu ya Biashara, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

***Tunakutakia kila la heri kwenye utekelezaji wa majukumu yako***

# Habari picha

Picha mbalimbali kwenye hafla ya kumkaribisha MUCE Prof. Deusdedit A. Rwehumbiza, Naibu Rasi - Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam.










Sweet Memories

HAPPY MOMENTS

